

## **TAARIFA YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI**

**MAHALI:** WIZARA YA NISHATI, DAR ES SALAAM

**TAREHE:** JUNI 5 2020

Total East Africa Midstream B.V. (TEAM BV) kampuni inayosimamia Mradi<sup>1</sup> wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)<sup>2</sup> imefanya kikao na Waziri wa Nishati nchini Tanzania Dr. Medard Kalemani kwa lengo la kuitaarifu Serikali maendeleo ya Mradi katika eneo la Ziwa Albert nchini Uganda pamoja na maendeleo ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Taarifa kuu iliyowasilishwa na kujadiliwa pamoja na Wizara ya Nishati ni matokeo ya makubaliano mapya na kampuni ya Tullow ya kununua hisa zake katika Mradi wa eneo la Ziwa Albert. TEAM B.V imaeleza Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Nishati kuwa hisa zote za Tullow zitanunuliwa na kampuni ya Total na kupelekea Kampuni ya Total kuwa na asilimia 66.7% katika hisa za mkondo wa juu na kampuni ya CNOOC kuwa na asilimia 33.3%.

Makubaliano haya na Tullow yataiwezesha Kampuni ya Total na CNOOC, kukamilisha kwa haraka makubaliano ya kisheria na ya kibiashara nchini Uganda na Tanzania ili kuwezesha kufikia Maamuzi ya Mwisho ya Uwekezaji (FID) na hatimaye utekelezaji wa Mradi.

Vilevile, Kampuni ya Total na Wizara ya Nishati wamezungumzia mipango ya kuendelea na mazungumzo ya Makubaliano ya Serikali husika (wenyeji), Makubaliano ya wabia/wanahisa, Pamoja na makubaliano ya maswala ya usafirishaji ili kuleta uwiano wa makubaliano yote kwa ajili ya kuendelea na Maamuzi ya Mwisho ya Uwekezaji (FID).

Zaidi, Kampuni ya Total imeitaarifu Wizara ya Nishati kuwa hali ya mabadiliko makubwa katika uchumi wa dunia italazimu kufanya maboresho katika ofa za zabuni mbalimbali za kimataifa ili kulingana na matakwa mapya katika soko.

TEAM B.V. imeishukuru Wizara ya Nishati na Serikali ya Tanzania kwa ujumla kwa ushirikiano wake mkubwa katika kuhakikisha mradi wa EACOP unafanikiwa na unaendelea kutekeleza lengo lake la kusimamia sheria za kitaifa pamoja na viwango bora vya utendaji vya kimataifa.

Bomba la Mafuta Ghafi litafungua fursa Afrika Mashariki kwa kuvutia wawekezaji. Mradi utapelekea kuwa na ongezeko la zaidi ya asilimia 60% ya Fedha za moja kwa moja za Kigeni (FDI) nchini Uganda na Tanzania katika kipindi cha ujenzi. Msingi wa mafanikio ya Mradi utapatikana kupitia ushirikiano mzuri na uelewano wa wadau wote.

---

<sup>1</sup> Huu ni Mradi unaoendeshwa na sekta binafsi kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania na Uganda.

<sup>2</sup> Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki linaundwa na bomba la inchi 24 linalotunza joto na kufunikwa ardhini, vituo sita vya kusukuma mafuta ( viwili viko nchini Uganda na vinne viko Tanzania), vituo viwili vya kupunguza kasi ya mafuta vyote viko nchini Tanzania pamoja na Kituo kwa ajili ya usafirishaji wa mafuta kilicho katika eneo la bahari. Mafuta ya Uganda yana asili ya uzito na hali ya nta hivyo kuhitaji mafuta hayo kusafirikwa katika kiwango cha nyuzi joto 50° ili yaweze kufikia kiwango cha kutiririka. Ilikuhakikisha bomba linakuwa na kiwango cha joto kinachohitajika, bomba litapashwa joto kwa njia ya umeme, na kulifanya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kuwa bomba refu zaidi duniani linalopashwa joto kwa njia ya umeme.



**-MWISHO-**

**Kwa taarifa zaidi au kufanya mahojiano kwa ajili ya vyombo vya habari tafadhali wasiliana nasi kupitia:**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano,  
Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi – Tanzania  
Mariagoreth Charles

**Simu ya ofisi:** +255 22 2214100/4102/4103  
**Simu ya mkononi:** +255 699 000 341  
**Baruapepe:** [mariagoreth.muangirwa@external.total.com](mailto:mariagoreth.muangirwa@external.total.com)  
**Tovuti:** [www.eacop.com](http://www.eacop.com)